



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAASISI YA UONGOZI

UONGOZI  
Institute

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

KITABU CHA MAISHA YA HAYATI EDWARD MORINGE SOKOINE  
KUZINDULIWA TAREHE 30 SEPTEMBER 2024

**28 Septemba, 2024:** Kitabu cha maisha ya Hayati Edward Moringe Sokoine, aliyejikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kitiwacho “Edward Moringe Sokoine: Maisha na Uongozi Wake” kinatarajiwa kuzinduliwa tarehe 30 Septemba 2024 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam.

Mgeni rasmi wa tukio hilo atakuwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wageni watajumuisha viongozi wakuu, viongozi waandamizi kutoka kwenye sekta za umma na binafsi, viongozi wastaafuli, mabalozi, na wawakilishi wa washirika wa maendeleo, taasisi za elimu ya juu, na asasi za kiraia.

Kitabu hiki, kilichoandaliwa na Taasisi ya UONGOZI kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, kinaangazia safari yake, kuanzia makuzi yake katika jamii ya Kimasai, hadi kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi, ikiwemo Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kinachangia kukuza historia ya Tanzania na Bara la Afrika kwa ujumla.

Baada ya uzinduzi, kitabu kitapatikana kwenye maduka ya vitabu na maktaba mbali mbali nchini, vile vile mtandaoni kupitia [www.mkukinanyota.com](http://www.mkukinanyota.com).

Ushiriki katika tukio hili ni kwa mwaliko pekee.

Imetolewa na,

Suzana Aroko

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma**